**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**

**TUME YA TAIFA YA UCHAGUZI**

# TAARIFA KWA UMMA KUHUSU ASASI ZA KIRAIA ZILIZOPATA KIBALI CHA KUTOA ELIMU YA MPIGA KURA WAKATI WA UCHAGUZI MDOGO WA UDIWANI KATIKA KATA 23 TANZANIA BARA

**Dodoma, 24 Februari, 2024**

Tume ya Taifa ya Uchaguzi katika kikao chake cha tarehe 24 Februari, 2024, imetoa vibali vya kutoa elimu ya mpiga kura wakati wa uchaguzi mdogo wa Udiwani katika kata 23 za Tanzania Bara kwa asasi za kiraia 11. Tume imefikia uamuzi huo kwa kuzingatia kanuni ya 3 ya Kanuni za Uchaguzi wa Serikali za Mitaa (Uchaguzi wa Madiwani) za mwaka 2020, inayoipa Tume jukumu la kutoa elimu ya mpiga kura nchi nzima, kuratibu na kusimamia taasisi na asasi za kiraia zinazotoa elimu hiyo. Orodha ya asasi za kiraia zilizopata kibali cha kutoa elimu ya mpiga kura na maeneo watakayotoa elimu hiyo, imeoneshwa katika jedwali lifuatalo:-

| NA. | JINA LA ASASI YA KIRAIA | HALMASHAURI | KATA |
|---|---|---|---|
| 1. | Mbogwe Legal Aid Organization (MBOLAO) | Halmashauri ya Wilaya ya Mbogwe | Isebya |
| 2. | Sustainable Hub for Policy Initiatives (SHPI)) | Halmashauri ya Manispaa ya Musoma | Mshikamano |
| | | Halmashauri ya Wilaya ya Butiama | Busegwe |
| 3. | Promotion and Women Development Association (PWDA) | Halmashauri ya Manispaa ya Kigoma/Ujiji | Kasingirima |
| 4. | Bagamoyo Community Capacity Empowerment and Education (BCCEE) | Halmashauri ya Wilaya ya Bagamoyo | Fukayosi |
| 5. | Action for Democratic Governance (A4DG) | Halmashauri ya Manispaa ya Kigamboni | Kimbiji |

| NA. | JINA LA ASASI YA KIRAIA | HALMASHAURI | KATA |
|---|---|---|---|
| 6. | Vanessa Foundation | Halmashauri ya Wilaya ya Kyela | Nkokwa |
| 7. | Tanzania Centre for Disability Development Initiatives (TCDDI) | Halmashauri ya Wilaya ya Kyela | Nkokwa |
| 8. | Safe Society Platform Tanzania (SSPT) | Halmashauri ya Wilaya ya Butiama | Busegwe |
| | | Halmashauri ya Wilaya ya Mbogwe | Isebya |
| 9 | Youth Against Aids and Poverty Association (YAAPA) | Halmashauri ya Manispaa ya Kigoma/Ujiji | Kasingirima |
| 10 | Musoma Municipal Paralegal Organisation (MMPO) | Halmashauri ya Manispaa ya Musoma | Mshikamano |
| 11 | Shirika la Elimu ya Uraia na Uzalendo "Civic Education and Patriotism Association" | Halmashauri ya Manispaa ya Kigamboni | Kimbiji |
| | | Halmashauri ya Mji Kibaha | Msangani |
| | | Halmashauri ya Wilaya ya Bagamoyo | Fukayosi |
| | | Halmashauri ya Wilaya ya Kibiti | Mlanzi |
| | | Halmashauri ya Wilaya ya Kilwa | Kibata |

Aidha, katika utekelezaji wa jukumu la kutoa elimu ya mpiga kura, asasi hizo zitapaswa kuzingatia Mwongozo wa Elimu ya Mpiga Kura wa Mwaka 2020 katika kipindi chote cha kutoa elimu hiyo katika uchaguzi mdogo.

Tume inatumia fursa hii kuzipongeza asasi zote za kiraia zilizopata kibali cha kutoa elimu ya mpiga kura. Vile vile, Tume inazikumbusha asasi za kirai zilizopata kibali cha kutoa elimu ya mpiga kura kuzingatia sheria, kanuni, maadili ya uchaguzi, taratibu, miongozo na maelekezo ya Tume katika kipindi chote cha uchaguzi.

Imetolewa na:

Kailima, R. K

**MKURUGENZI WA UCHAGUZI**